

MAJIBU YENYE FAIDA

NO.10

KUHUSU

MASWALI YA MIFUMO MIPYA

MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN ALFAWZAN

MFASIRI : UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO

PONGWE -TANGA - TANZANIA

Swali la kumi na tatu:

**Je..!Anayejiita salafiy atazingatiwa ni Hizbiy
(mwanachama wa kikundi fulani)?**

Jawabu: Kujiita salafiy kukiwa ni kwa hakika (kweli) basi hakuna ubaya kujiita huko,ama yakiwa ni madai tu basi haitafaa kujiita salafiy na hali ya kuwa mtu huyo hayuko katika njia (manhaj) ya wema waliyotangulia,na Ashaairah kwa mfano:Wanasema:Sisi Ahlu-s-sunna waljama'ah, na jambo hili (kauli hii) si sahihi, kwa sababu yale ambayo wako nayo hayakuwa manhaj (mfumo) wa Ahlu-s-sunnah waljama'ah,halikadhalika Mu'tazilah wanajiita wenyewe "**Muwahhiduuna**" (wenye

tawhidi eti wanampwekesha Allah kwa madai yao..!).

*Kila mmoja anadai ana mafungamano na Leyla,
Na Leyla hawakubalii hayo (mafungamano).*

Basi yule ambaye anadai kwamba yeye yuko kwenye mwenendo wa Ahlu-s-sunna waljama'ah, basi (bila shaka) atafuata njia ya Ahlu-s-sunnah waljama'ah na atawaacha(mukhaalifuun) wenyewe kwenda kinyume (na njia hiyo). Ama kuwa yeye anataka akusanye baina ya “Mburukenge na Chewa (samaki) kama wanavyosema waarabu, yaani anataka akusanye kati ya wanyama wa jangwani na wanyama wa baharini hili halitawezekana, au anataka akusanye baina ya

moto na maji katika kitunga (kikapu) kimoja..!
haikusanyiki madhehebu ya Ahlu-s-sunnah
waljama'ah pamoja na madhehebu yenye
kuwakhalifu wao,kama makhawariji (waasi
wenye kuwapinga watawala) na Mu'tazilah,na
mahizbiy katika wale ambao wanawaita
“waislamu wa leo wenze kwenda na wakati” na
huyu (muislamu wa leo mweye kwenda na
wakati) ndiye ambaye anataka kukusanya
upotevu wa watu wa zama hizi pamoja na njia
ya wema waliyotangulia.

Basi **“Hautatengemaa umma huu isipokuwa kwa
kile ambacho kimewatengeneza wale wa
mwanzo wa umma huu.”**

Alhassil ni kwamba,hakuna budi kupambanua
mambo na kuyachuja.